# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL1

# KISWAHILI PAPER 1 ANSWERS

**1.** **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA 102/1**

**–INSHA 1**. Hili ni swali la hoja. Mambo muhimu ya kuzingatia ni:

a) Sura

(i) Kichwa/mada/anwani ya tahadhari.

(ii) Tarehe ya kuandikwa kwa tahadhari.

(iii)Sahihi ya mwandishi.

(iv) Jina la mwandishi

(v) Cheo cha mwandishi.

(b) Maudhui. Baadhi ya hoja ni:

i) Namna mazingira yalivyoharibiwa.

- Ukataji ovyovyo wa miti.
- Uchomaji wa makaa.
- Uteketezaji wa misitu.
- Utupaji ovyo wa karatasi za plastiki.
- Kulima kwenye miinuko na kando ya chemichemi za maji.
- Matumizi ya vyoo vya kupeperushwa.
- Mioshi kutoka viwandani.
- Maji taka kutoka viwandani kuelekezwa mitoni.
- Unyunyiziaji wa kemikali sumu kwa mimea inayokuzwa kando ya mito.
- Ufugaji wa idadi kubwa ya mifugo katika sehemu udogo ya ardhi.
- Miziki yenye sauti za juu kutoka kwenye vilabu na mikahawa.

(ii) Hatua za kuchukuliwa kwa wanaoharibu mazingira.

- Kukamatwa na kufunguliwa mashtaka.
- Kutozwa faini.
- Wakataji miti lazima wawe na kibali.
- Maafisa wa afya wafanye ukaguzi kuhakikisha wakaazi wamechimba/wametengeneza vyoo.
- Walinzi wa sehemu za miinuko na chemichemi za maji wataajiriwa
- Viwanda visivyodumisha uhifadhi wa mazingira vitapokonywa leseni zao.

- Mikahawa na vilabu vyenye miziki ya sauti za juu vitafungwa.

- Sheria itapitishwa kuhusu idadi ya mifugo wanaofaa kuwekwa katika sehemu Fulani ya ardhi.

**2.** **Tanbihi:**
**Mtahini akadirie hoja nyingine zozote zilizo sahihi.** .

Hili ni swali la hoja. Hoja za mtahiniwa zilenge kubainisha kuwa ufisadi ni janga la kitaifa. Baadhi ya hoja ni:

i) Unyakuzi wa ardhi.

(ii) Nafasi za kazi kutolewa kwa njia za kifisadi kama vile jeshini,idara ya polisi,huduma ya vijana kwa taifa.

(iii)Maafisa wakuu serikalini kuiba mabilioni ya pesa.

(iv) Askari wa trafiki kupokea hongo kutoka kwa madereva wasiotimiza sheria za uendeshaji wa magari.

(v) Nafasi katika shule na vyuo kutolewa kwa wale wenye pesa/utajiri.

(vi) Huduma katika hospitali za umma kudorora kutokana na madaktari kuiba dawa na vifaa vingine vya matibabu.

(vii) Kesi Mahakamani kuamuriwa kwa misingi ya utajiri au ufukara alionao mhukumiwa.

(viii) Wagombezi wa kisiasa hutumia fedha nyingi kuwahonga wapiga kura wakati wa kampeni za uchaguzi.

(ix) Maafisa wa Baraza la mitihani la kitaifa hushiriki katika uuzaji wa nakala za mitihani kwa wazazi na wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mtihani huo.

(x) Kupandishwa mamlaka katika mashirika ya umma nay a kibinafsi hutegemea kiwango cha hongo anachokitoa anayetarajia kupandishwa cheo.
.

3. **Hili ni swali la methali**.
- Si lazima mtahiniwa aeleze maana ya juu na ya ndani.

- Methali hii ina sehemu mbili kuu

- (i) Kupigana kwa fahali.

(ii) Kuumia kwa nyasi. Jibu la mtahiniwa lilenge sehemu zote mbili. Mfano:

Kisa cha mtahiniwa kidhihirishe kuwa watu wawili au Zaidi wenye uwezo wanapozozana au kupigana,waumiao ni wale wanyonge.

4. Hii ni insha ya mdokezo.
- Mtahiniwa atumie maneno aliyopewa kutanguliza kisa chake.
- Kisa chake chaweza kulenga tukio halisi au tendo la ndotoni. Mfano: Mhusika aliyezama katika usingizi mzito au aliye karibu kuchelewa kwa shughuli Fulani anapoamshwa na mamaye/shangaziye/mwanawe/rafikiye.

**Tanbihi**:

Mwongozo huu utumike sambamba na wa kudumu katika kumkadiria/kukadiria kazi ya mtahiniwa.

**USAHIHISHAJI**

Karatasi hii imedhamiria kutahini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, wenye utiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia: Ubainifu mwingi, na hati nadhifu. Kutegemea maagizo ya swali. lenyewe na umahiri wa lugha, ni Iazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtahini Iazima asome insha yote ili aweze kukadiria viwango mbalimbali vilivyopendekezwa, yaani A, B,C ama D kutegemea mahali popote pale pafaapo kuikadiria insha ya mtahihiwa.

**KIWANGO CHA D-MAKI 01-05**

1. Insha ya aina hii haileweki kwa vyovyote, ama uwezo wa mtahiniwa kutumia lugha ni hafifu sana hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa .hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika, uakifishaji usiofaa na insha ina mskosa ya kila aina ya kisarufi, kimaendelezo mtindo mbovu n.k.

**VIWANGO TOFAUTI VYA D**

D-(Kiwango cha chini) maki 01-02 Insha hainampangilio maalum, na haieleweki kwa vyovyote vile. Kwa mfano, kunakili swali au kujitungia swali na kulijibu.

D (Wastani)-Maki 03 Utiririko wa mawazo haupo-na insha haieleweki. Makosa ni

D+ (Kiwango cha juu) Maki, 04-05 Ingawa insha hii ina lugha dhaifu ya Kiswahili na makosa mengi ya kila aina, unaweza .kutambua kile ambacho anajaribu.kuwasilisha **KIWANGO CHA C**

–Maki 06-10 Kiwango hiki kina makosa yafuatayo:

1. Mtahiniwa anaweza kuwasilisha mawazo yake.lakini kwa njia hafifu. kamilifu.

2. Hana uhakika wa matumizi ya lugha.

3. Mada huwa haikukuzwa au kuendelezwa kikamilifu.

4. Mtahiniwa anaweza kupotoka hapa na pale.

5. Kujirudiarudia ni dhahiri.

6. Mpangilio wake wa kazi ni hafifu na hauna mtiririko.

7. Hana matumizi mazuri ya lugha.

8. Mtahiniwa ana athari za lugha ya kwanza ambayo huonekana dhahiri kama vile "papa" badala ya "baba" "chakura" badala ya "chakula”Juki" badala “chuki", "tata" badala ya "dada'n.k

**VIWANGO TOFAUTI VYA C**

C-Kiwango cha chini)-Maki 06-07

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha mawazo yake

. Hana msamiati wala muundo wa sentensi mwafaka.

3. Ana makosa mengi ya msamiati,hijai na matumizi mabaya ya sarufi.

**C (wastani)-Maki08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.

2. hufanya makossa mengi ya sarufi

3. Hana ubunifu wa kutosha

4. Katika sentensi ndefu uakifishaji wake ni mbaya.

5. Ana makosa kadha ya hijai na msamiati.

**C+ (kiwango cha juu) –Maki 09-10**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri lakini kwa njia isiyo na mvuto

2. Dhana tofauti hazijitokezi kikamilifu.

3. Hutumia.misemo methali, tashibihi, tanakali za sauti n.k kwa njia isiyofaa

4. Utiririko wa mawazo bado haujitokezi wazi

5. Kuna makosa machache ya sarufi na hijai

**KIWANGO CHA B**
**-** Maki 11-15

1. Katika kiwango hiki,mtahiniwa anaonyesha. kuimudu .lugha viliyyo

2. Mtahiniwa hudhihirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujielieza

3. Hutumia miundo tofauti tofauti.ya sentensi vizuri.

4. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha kama vile kuandika sentensi-kwa njia tofauti tofauti na zikaleta maana sawa.

**5.** Mada huwa imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu. **VIWANGO TOFAUTI VYA B**

B-(Kiwango cha chini)-Mali 11-12

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa kuonyesha hoja tofauti, tofauti

2. Kuna utiririko mzuri wamawazo

3. Ana uwezo wa. Kutumia miundo tofauti tofauti yasentensi

4. Makosa ni machache.

**B (Wastani)-Maki 13**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha

. Anawasilisha ujumbe wake waziwazi kwa mawazo yanayodhihirika.

3. Matumizi ya lugha ya mnato huweza kudhihirika

4. Anatumia mifano michache ya msamiati mwafaka

5. Matumizi ya tanathali za semi yanaanza kudhihirika

6. Makosa machache ya hapana pale

**B+ (Kiwango cha iuu) Maki 14-15**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika

2. Mtahiniwa awasilisha ujumbe wake kwa njia inayovutia na kwa urahisi

3. Kuna makosa ya hapa na pale ambayo mtahiniwa hakudhamiria kuyafanya

4. Uteuzi wake wa msamiati.ni mzuri

5. Sarufi yake ni nzuri 6. Uakifishaji wake nimzuri

**KIWANGO CHA A (Maki 16-20)**

1. Mtahiniwa hudhihirisha ukomavu wa lugha. Ana utiririko mzuri wamawazo kulingana na mada

. Huzingatiamatumizi mazuriyamsamiati na sarofi

3. Makosa ya kawaida ya lugha ni machache

**VIWANGO TOFAUTI VYA A**

A-Kiwango cha chini) Maki 16-17

1. Mtahiniwa hudhihirisha ukomavu wa lugha.

2. Ana utiririko mizutri wa mawazo kulingana na mada.

3. Anapamba lugha kwa kutumia tamathali za usemi

4. Anazingatia matumizi mazuri ya msamiati na sarufi

5. Uakifishaji wake ni mzuri Zaidi.

6. Makosa machache ya hapa na pale

**A (Wastani)-Maki 18**

1. Mawazo yanadhihiriks zaidi.

2. Makossa ni machache mno.

3. Hutumia lugha ya mnato.

4. Hutumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia.

5. Sarufi yake ni nzuri.

6. Hutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.

7. Hujieleza kikamilifu

**A+ (Kiwango cha juu)-Maki 19-20**

. Mtahiniwa huwasilisha ujumbe kulingana na mada.

. Kutirirsha mawazo yake vizuri Zaidi.

. Hujieleza kikamilifu bila shida.

4. Hutoa hoja zilizokomaa

5. Makossa ni machache sana.

6. Masamiati wake ni hali ya juu.

| KIWANGO | ALAMA | MAKI |
|---|---|---|
| A | A-<br>A<br>A- | 19-20<br>18<br>16-17 |
| B | B+<br>B<br>B- | 14-15<br>12-13<br>11 |
| C | C+<br>C<br>C- | 09-10<br>08<br>09-10 |
| D | D+<br>D<br>D- | 04-05<br>03<br>01-02 |

**Jinsi ya kutuza mbalimbali**

1. Mtahiniwa asipozingatia sura ya insha aondolewe maki baada ya kutuzwa.

2. Mitindo ya uandishi isiingilie sana utahini

3. Hati ya mtahiniwa isitiliwe maanani mno Sarufi

1. Sahihisha kwa makini sana ukionyesha makosa yote yanayotokea.Makosa ya sarufi huwa katika:

2. Kuakifisha vibaya,kwa mfano,vikono,vituo,alama ya kuulizia n.k

3. Kutumia herufi ndogo au kubwa mahali si pake

4. Matumizi mabaya ya ngeli na viambishi,nyakati,vihusiano,muundo mbaya wa sentensi na mnyambuliko wa vitenzi na majina

5. Kuacha ayu kuongeza neno katika sentensi,kwa mfano.'kwa kwa.

6. Matumizi ya herufi kubwa Tazama: Matumizi ya herufi kubwa

(a) Mwanzo wa sentensi.

(b) Majina ya pekee.

(c) Majina ya mahali,miezi,nchi.

d) Mashirika,masomo,vitabu n.k

(e) Makabila,lugha n.k.

(f) Jina la Mungu.

(g) Majina ya kutambulisha

**Makosa ya hijai**

Haya ni makosa ya maendelezo.

Sahihisha huku ukiyaonyssha yanapotokea mara ya kwanza.

Makosa ya tahajiakuwa katika:

1. Kutenganisha neno kama vile 'aliye kuwa'

2. Kuunganisha maneno kama vile 'kwasababu'

3. kukata:silablvibaya kama vile 'ngan-o' Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama 'mahari' badala ya 'mahali'

4. Kuacha herufi katika neno kama 'aliekuja' badala ya 'aliyekuja'

5. Kuongeza herufi katika neno kama 'piya' badala. 'pia'

6. Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika herufi,

7. Kutoandika kistari cha kuunganisha neno ufikiapo pambizo au mwisho kuandika mahali si pake

8. Kuandika kistari pahali pasipofaa

9. Kuacha ritifaa au kuiweka pasipofaa

10. Kuandika maneno, 'kwakifupi mfano k.m n,k. v. v.

**Mtindo Mambo yatakayochunguzwa:**

1. Mpangilio wa kazi kiaya

2. Utiririko wa mawazo

3. Hati nzuri inayosomeka kwa urahisi

4. Namna anavyotumia methali,misemo,tamathali, za usemi na.mengmeyo

5. Unadhifu wa kazi

6. Kuandika herufi vizuri km. Jj, Pp, Uu, Mm, Kk,

7. Sura ya insha k.m barua, kumbukumbu, mahojiano mazimgunizo, ripoti, n.k Msamiati Jumla ya maneno yaliyotumiwa kiafikiana na mada au kichwa kilichopendekezwa. Maudhui na msamiati Baada ya kusoma mtungo utafikiria maudhui na msamiati uliomo kwa jumla Alama za kusahihishia =Hupigwa chini ya sehemu ambayo kosa la sarufi Irmetokeza kwa mara ya kwanza

-Hupigwa chini ya sehemu auneno ambako kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

^Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno √Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe. Maelezo mafupi

kuhusu tuzo la mtahini yanahitajika kila ukurasa uwe na alama ya chini katika kuonyesha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo. (alama 1)

**Urefu:**

Insha ya pili ikadiriwe kulingana na urefu au idadi ya maneno yaliyopendekezwa.Ikiwa mtungo huu haukufikia unaotakikana, mtahiniwa atatuzwa kulingana na urefu wa mtungowake:Maneno katika mstari:

**MANENO:**

Maneno 8-kurasa 1¾

Maneno 7-kurasa 2

Maneno 6-kurasa

Maneno 5-kurasa 2¾

Maneno 4-kurasa 3¾

Maneno 3-kurasa 4½